- Eleza kila kitu unachojifunza na mtoto wako. ongeza shughuli kama kupima urefu, uzito, na shinikizo la damu, pamoja na matarajio ya kuondoa viatu au kubadili nguo.
- Kuna video na picha kwa ajili ya mitihani na miadi mingi ya kawaida.
- Uliza mtoto wako kama anahisi yuko tayari, au kama anataka kukagua hatua tena.
- Himiza mawasiliano na utatuzi wa matatizo.

Ikiwa unajua hatua za miadi, zipitie kwa utaratibu na mtoto wako. Andika “ukweli” kuhusu hali hiyo - “Mambo ya ukweli” kuhusu hali hiyo - yale ambayo ni mazuri kwa mtoto wako, na yale ambayo yanaweza kuonekana kwa mtazamo hasi.

- Muulize mtoto wako anafikiri sehemu rahisi ya ziara itakuwa nini. Wasifu kwa ujasiri wao wa kushiriki katika sehemu hizo za uteuzi.
- Waulize wanafikiri ni sehemu gani itakuwa ngumu zaidi kwa miada. Shirikiana na mtoto wako ili kujua kile anachoweza kufanya ili kurahisisha sehemu ngumu. Hii inaweza kujumuisha kuleta vitu vichache vya starehe kutoka nyumbani, au kukaa kwenye mapaja yako.
- Mhimize mtoto wako kila mara kuuliza maswali na kueleza hisia au wasiwasi wake! Hizi ni fursa kwao kujua ni nini kita fanya mambo kuwa bora zaidi.

Panga shughuli au zawadi ya kufurahisha baada ya ziara.

- Mpe mtoto wako baadhi ya chaguo za shughuli za kufurahisha ambazo anaweza kufanya baada ya ziara - kwa mfano, kwenda kula chakula cha mchana, kutembelea bustani, au kucheza na mchezo maalum.
- Jumuisha hili katika hatua hunazopitia na kufanya mazoezi.
- Wakati wa ziara, wakumbushe kwamba kitu cha kufurahisha kinakuja baada ya kumaliza.

Hudhuria na mtoto wako wakati wa ziara.

- Wakati wa ziara, msifu mtoto wako anapopita hatua za ziara.
- Wakumbushe ni hatua zipi ambazo tayari wamekamilisha, na hatua gani zinakuja.
- Wahimize kuuliza maswali, kuomba mapumziko mafupi, au chombo cha kushughulikia. Kwa mfano, baadhi ya watoto hupenda mtoa huduma kuhesabu hadi tatu kabla ya kutoa damu au kudunga sindano. Mhimize mtoto wako kuomba hii, ikiwa ni kile anachotaka.
- Mwambie mtoto wako kwamba unajivunia kwa kufuata maelekezo.

The Doctor's Visit

Visiting the doctor often is important for your child's health and wellness. When at your appointment, remember that all people with a disability should determine their needs, or a family should determine the needs of a child. Including:

- ✓ Choosing and setting their own goals
- ✓ Being involved in making life decisions
- ✓ Self-advocating
- ✓ Working to reach their goals

At appointments for babies and children under age 6, you will be asked to answer questions like "Does your baby notice when you are speaking to them? Does your baby have trouble seeing you?" These questions help a doctor know if your child is growing well what their strengths are. They are part of the "Ages and Stages Questionnaire." You will either be asked these questions by a provider, or be asked to answer them while you wait for your doctor.

The Ages and Stages Questionnaire:

- *Shows families and providers where there are specific strengths and skills*
- *Helps families and providers identify where they may be gaps*
- *If your child is not meeting their developmental milestone, such as being able to hold their head up or walk, the provider will refer you to someone to help out*

Ziara kwa Daktari

Kutembelea daktari mara kwa mara ni muhimu kwa afya na ustawi wa mtoto wako. Wakati wa miadi yako, kumbuka kuwa watu wote wenye ulemavu wanapaswa kujua mahitaji yao, au familia inapaswa kujua mahitaji ya mtoto. Hii ni pamoja na:

- ✓ Kuchagua na kuweka malengo yao wenyewe
- ✓ Kushiriki katika kufanya maamuzi ya maisha
- ✓ kujitetea
- ✓ Kufanya kazi ilikufikia malengo yao

Katika miadi kwa watoto wachanga na chini ya miaka 6, utaulizwa maswali kama “Je! Mtoto wako anatambua unapozungumza nao? Je! Mtoto wako ana shida kukuona?” Maswali haya husaidia daktari kujua ikiwa mtoto wako anakua vizuri na ana uwezo gani. Hizi Ni sehemu za “Maswali za Umri na Hatua.” Utaulizwa maswali haya na mtoa huduma, au utaulizwa kuyajibu wakati unasubiri daktari wako.

Maswali ya Umri na Hatua:

- *Huonyesha familia na watoa huduma wapi kuna nguvu na ujuzi maalum*
- *Husaidia familia na watoa huduma kutambua ni wapi wanaweza kuwa na mapungufu.*
- *Ikiwa mtoto wako hafikii hatua yake ya ukuaji, kama vile kuweza kuinua kichwa au kutembea, mtoa huduma atakuelekeza kwa mtu wa kukusaidia.*

Get the Help You Need For Your Child with a Disability

If your child needs help, the doctor will send you to people called "specialists" who will help you.

1. **Ask your child's doctor to provide a referral to developmental pediatrics.** This person has special skills to help your child if they need extra help whether it's with talking, hearing, walking or more.

2. **Ask them where you can take the referral for help.** Write down the name and phone number of someone you can call.

3. **Call the number the doctor gives you** to get your child special help.

Contact these people if you need help—they can call you back with a translator:

- For children ages 0-6, **Help Me Grow 1 (833) 868-4769** or **email them at hello@helpmegroworegon.org**
- For children over age 6, **Providence Swindells Resource Center at (503) 215-2429**
- For children and youth ages 0-26 **Oregon Family to Family Health Information Center. 1 (855) 323-6744**

DEFINITIONS

What does it mean if you get a **referral**? A referral is when a doctor will send you to someone who has the skills to help your child with their disability. For example, your doctor may give your child a referral to a speech therapist. A speech therapist is someone who can help your child with speech if they are slow to begin speaking or are hard to understand for their age. A referral can be a piece of paper, or you may be asked to call the specialist. Sometimes, you will need to wait for the specialist to call you. A referral can take a few days, or a few weeks. Ask how long you can expect to wait for an appointment.

Pata Msaada Unao Hitajika kwa Mtoto Wako Mwenye Ulemavu

Ikiwa mtoto wako anahitaji msaada, daktari atakutuma kwa watu wanaoitwa “wataalamu” ambao watakusaidia.

1. **Uliza daktari wa mtoto wako akupe rufaa kwa Daktari wa watoto kwa maendeleo.** Mtu huyu ana ujuzi maalum wa kusaidia mtoto wako ikiwa wanahitaji usaidizi wa ziada, iwe ni kwa kuzungumza, kusikia, kutembea au zaidi.
2. **Waulize ni wapi unaweza kuchukua rufaa kwa usaidizi.** Andika jina na nambari ya simu ya mtu unayeweza kupiga.
3. Piga simu nambari ambayo daktari anakupa ili kupata msaada maalum kwa mtoto wako.

Wasiliana na watu hawa ikiwa unahitaji usaidizi - wanaweza kukupigia simu na mkalimani:

- Kwa watoto wenye umri kati ya 0-6, Help Me Grow **1 (833) 868-4769** au barua pepe kwa **hello@helpmegroworegon.org**
- Kwa watoto wenye umri zaidi wa miaka 6, **Providence Swindells Resource Center kwa (503) 215-2429**
- Kwa watoto na vijana wenye umri kati ya 0-26, **Kituo cha Habari za Afya ya Familia ya Familia ya Oregon. 1 (855) 323-6744**

MAELEZO

Ina maanisha nini kupata rufaa? Rufaa ni wakati daktari anakutuma kwa mtu ambaye ana ujuzi wa kumsaidia mtoto wako na ulemavu wake. Kwa mfano, daktari wako anaweza kumpatia mtoto wako rufaa kwa mtaalamu wa hotuba. Mtaalamu wa hotuba ni mtu anayeweza kumsaidia mtoto wako kwa hotuba ikiwa anachelewa kuanza kuzungumza au ni vigumu kuelewa kwa umri wake. Rufaa inaweza kuwa kipande cha karatasi, au unaweza kuulizwa kumwita mtaalamu. Wakati mwingine, utahitaji kusubiri mtaalamu akupigie simu. Rufaa inaweza kuchukua siku chache, au wiki chache. Uliza ni muda gani unaweza kutarajia kusubiri miadi.

Your Care Team

There are all kinds of people who can help you to teach your child everything they need to live their daily lives with strength. They can help your child become independent as much as possible. Some of the names of these people are:

Your Doctor

A Primary Care Provider is the first person you will visit at a clinic to help support your child and tell you all the things you need to know about how they are growing.

Care Coordinator/Nurse

helps you to manage all the referrals and specialists you get.

Occupational Therapist

helps your child develop, recover, or maintain the skills needed for daily living and working. They can help your child at school or in the community.

Physical Therapist

help your child with their movement.

A Behavioral Therapist

can help your child with their feelings and emotions and teach them skills and practices to help manage big feelings.

A Speech Therapist

can help if you child has difficulties with communication, eating, drinking and swallowing.

If you need **special food or medicines** for your child, these terms are helpful:

Medical Foods

Equipment provider

Pharmacy

Make sure you right down the names and numbers of all the people you work with so you can keep track of the support network for your child.

Timu Yako ya Utunzaji

Kuna kila aina ya watu ambao wanaweza kukusaidia kumfundisha mtoto wako kilakitu anachohitaji ili kuishi maisha yao ya kila siku kwa nguvu. Wanaweza kumsaidia mtoto wako kujitegemea iwezekanavyo.

Baadhi ya majina ya watu hawa ni:

Daktari wako

Mtoa Huduma ya Msingi ndiye mtu wa kwanza utakayemtembelea kwenye kliniki ili kusaidia kumsaidia mtoto wako na kukuambia mambo yote unayohitaji kujua kuhusu jinsi anavyokua.

Mratibu/Muuguzi

hukusaidia kudhibiti marejeleo yote na wataalamu unaopata kwa Huduma.

Mtaalamu wa Tiba Shughuli

husaidia mtoto wako kuendeleza, kupona, au kudumisha ujuzi unaohitajika kwa maisha ya kila siku na kazi. Wanaweza kumsaidia mtoto wako shuleni au katika jamii.

Mtaalamu wa Tiba ya Viungo

husaidia mtoto wako na harakati zao.

Mtaalamu wa Tiba ya Tabia

anaweza kumsaidia mtoto wako na hisia na mwenendo wao na kuwafundisha ujuzi na mbinu za kusaidia kudhibiti hisia kubwa.’

Mtaalam wa Kuzungumuza

anaweza kusaidia ikiwa mtoto wako ana shida na mawasiliano, kula, kunywa, na kumeza.

Ikiwa unahitaji chakula maalum au dawa kwa mtoto wako, misemo hii ni muhimu:

Vyakula vya Matibabu

Mtoa Vifaa

Duka la dawa

Hakikisha umeandika chini kabisa majina na nambari za watu wote unaofanya nao kazi ili uweze kufuatilia mtandao wa usaidizi wa mtoto wako.

The School Visit

While going to the doctor gives you help for your child's body and mind to learn how to be in the everyday world, the schools help your children learn to read, write, do math and more. A disability does not prevent a child from learning. They just need support. The education they receive is called "special education." After you get help at the doctor's, you will need to get help for your child at school when they start to go to school. You can call or visit the school and tell them your child has a disability. You can tell them you need special education, and they will help you create a team to help your child.

As a part of this education, your child will be assigned someone to help them in school and help you make a plan for their learning called an "individual education plan" or IEP. Parents have a very important role in the team that supports their child and should be included in all decisions. When you make the IEP document with the school team, there is a section asking parents to share other ideas and concerns. It is important to bring a written document with your ideas, concerns, and solutions to each IEP meeting. Share your document with the team and refer to it often. As your child grows older they will become part of this planning team.

These are the names of people who will help you:

- **Teacher**
- **School Nurse**
- **Special Education Coordinator**

Here are some places that can help you:

- **FACT Oregon** helps families understand the steps to helping a child with a disability. **(503) 786- 6082**
- **Help Me Grow** is a free and confidential family support line that provides seamless access to community services. You can call them at **1 (833) 868-4769** or email them at **hello@helpmegroworegon.org**
- The **Oregon Department of Education** can help answers about any school district. You can email them at **ode.specialeducationquestions@ode.oregon.gov** or by phone at **(503) 947-5600**. Make sure to include your child's school district to help them connect you with a staff member who can help.

TIPS FOR PARENTS

- ✓ You may have to call more than once
- ✓ The process can take a long time
- ✓ You will be assigned a services coordinator. Keep their information handy.

Ziara ya Shule

Wakati wa kwenda kwa daktari hukupa msaada kwa mwili na akili ya mtoto wako kujifunza jinsi ya kuwa katika ulimwengu wa kila siku, shule huwasaidia watoto wako kujifunza kusoma, kuandika, kufanya hesabu na zaidi. Ulemavu hauzuili mtoto kujifunza. Wanahitaji tu msaada. Elimu wanayopata inaitwa "elimu maalum." Baada ya kupata msaada kwa daktari, utahitaji kupata msaada kwa mtoto wako shuleni atakapoanza kwenda shule. Unaweza kupiga simu au kutembelea shule na waambie mtoto wako ana ulemavu. Unaweza kuwaambia unahitaji elimu maalum, na watakusaidia kuunda timu ya kumsaidia mtoto wako.

Kama Sehemu ya elimu hii, mtoto wako atapewa mtu wa kumsaidia shuleni na kukusaidia kupanga mpango kwa masomo yao unayoitwa "mpango wa elimu ya mtu binafsi" au IEP. Wazazi wana jukumu muhimu sana katika timu hiyo inasaidia mtoto wao na inapaswa kujumuishwa katika maamuzi yote. Unapotengeneza hati ya IEP na timu ya shule, kuna sehemu inayowataka wazazi kushiriki mawazo na mahangaiko mengine. Ni muhimu kuleta hati iliyoandikwa na mawazo yako, wasiwasi, na ufumbuzi kwa kila mkutano wa IEP. Shiriki hati yako na timu na uirejelee mara kwa mara. Mtoto wako anapokua, mkubwa atakuwa sehemu ya timu hii ya kupanga.

Haya ndio majina ya watu ambao watakusaidia:

- **Mwalimu**
- **Muuguzi wa Shule**
- **Mratibu wa Elimu Maalum**

Hapa kuna baadhi ya maeneo ambayo yanaweza kukusaidia

- **FACT Oregon** husaidia familia kuelewa hatua za kumsaidia mtoto mwenye ulemavu. **(503) 786-6082**
- **Help Me Grow Help Me Grow** ni laini ya usaidizi ya kifamilia isiyolipishwa na ya siri ambayo hutoa ufikiaji wa huduma za jamii bila mshono. Unaweza kuwapigia simu kwa **1 (833) 868-4769** au kuwatumia barua pepe kwa **hello@helpmegroworegon.org**
- **Idara ya Elimu ya Oregon** inaweza kusaidia kujibu maswali kuhusu wilaya yoyote ya shule. Unaweza kuwatumia barua pepe kwa **ode.specialeducationquestions@ode.oregon.gov** au kupitia simu kwa **(503) 947-5600.** Hakikisha kuwa umejumuisha wilaya ya shule ya mtoto wako ili kumasaidia kukuunganisha na mfanyikazi anayeweza kuwasaidia.

VIDOKEZO KWA WAZAZI

✓ Huenda ukahitaji kupiga simu zaidi ya mara moja

✓ Mchakato unaweza kuchukua muda mrefu

✓ Utapangiwa mratibu wa huduma. Hifadhi habari zao karibu

Developmental Disability Services

You can also get help from an office called Developmental Disability Services.

You will get a **Developmental Disabilities Case Manager (*Kiis Maareeyaha Naafada Koriimada*)** who will meet with each person to review their current situation, identify needs, and make referrals for essential services.

They do the following:

- Work and advocate for you
- Meet, assess your child's needs and help you understand and access available services and supports
- Create an Individualized Service Plan (ISP) to help your child lead a happy, healthy and fulfilling life
- Connect you with community provider agencies
- Monitor, provide resources and assist with your child's health, safety and ISP implementation.
- They will provide you with a case manager who should meet with you often to help with services
- If you need anything to help your child, they can help get it for you. For example, you might have a child who is visually impaired that might need a special computer or home or a child might need a wheelchair.

For more information call:

Multnomah County Main Office

Office Hours:
Monday–Friday, 8am–5pm

Phone: (503) 988-3658

After Hours Help Line:
(503) 988-3646

Washington County Main Office

Office Hours:
Monday–Friday, 8am–5pm

Phone: (503) 846-3150

Clackamas County Main Office

Office Hours:
Monday–Thursday, 7am–6pm

Phone: (503) 655-8640

Huduma Za Ulemavu Wa Kimaendeleo

Unaweza pia kupata msaada kutoka kwenye ofisi inayoitwa Huduma za Ulemavu wa Kimaendeleo.

Utapata Meneja wa Kesi za Ulemavu wa Kimaendeleo ambaye atakutana na kila mtu kuchunguza hali yao ya sasa, kutambua mahitaji, na kufanya rufaa kwa huduma muhimu.

Wanafanya yafuatayo:

- Kufanya kazi na kukutetea
- Kukutana, kutathmini mahitaji ya mtoto wako na kukusaidia kuelewa na kupata huduma na msaada uliopo
- Kuunda Mpango wa Huduma Binafsi (ISP) kusaidia mtoto wako kuishi maisha yenye furaha, afya na yenye kuridhisha
- Kukuunganisha na mashirika ya huduma ya jamii
- Kufuatilia, kutoa rasilimali na kusaidia katika afya, usalama na utekelezaji wa ISP ya mtoto wako.
- Watakupatia msimamizi wa kesi ambaye anafaa kukutana nawe mara kwa mara kukusaidia na huduma
- Ikiwa unahitaji kitu chochote kumsaidia mtoto wako, wanaweza kukusaidia kukipata. Kwa mfano, unaweza kuwa na mtoto ambaye ni mlemavu wa macho ambaye anaweza kuhitaji kompyuta maalum au nyumba au mtoto anaweza kuhitaji kiti cha magurudumu.

Kwa maelezo zaidi piga simu:

Multnomah County Ofisi Kuu

Masaa ya Kazi:
Jumatatu–Ijumaa,
8 asubuhi–5 jioni

Simu: (503) 988-3658

Mstari wa Msaada baada ya Masaa:
(503) 988-3646

Washington County Ofisi Kuu

Masaa ya Kazi:
Jumatatu–Ijumaa,
8 asubuhi–5 jioni

Simu: (503) 846-3150

Clackamas County Ofisi Kuu

Masaa ya Kazi:
Jumatatu–Alhamisi,
7 asubuhi–6 jioni

Simu: (503) 655-8640

The American Disabilities Act

As a parent of a child with a disability, there is a law that will protect them and you called the American Disabilities Act. It is a law the federal government of the United States made to make sure people with disabilities are treated fairly. The ADA prohibits discrimination on the basis of disability just as other civil rights laws prohibit discrimination on the basis of race, color, sex, national origin, age, and religion. The ADA guarantees that people with disabilities have the same opportunities as everyone else to enjoy employment opportunities, purchase goods and services, and participate in state and local government programs

If you feel like someone isn't treating you or your child with a disability fairly or your child is being harmed or bullied, you can call this number for help:

ADA Information Line: 1 (800) 514-0301 or **1 (833) 610-1264 (TTY)**

- Monday, Tuesday, Wednesday, Friday, 9:30am–12pm and 3–5:30pm ET
- Thursday, 2:30–5:30pm ET

Sheria ya Walemavu ya Marekani

Kama mzazi wa mtoto mwenye ulemavu, kuna sheria itakayowalinda wao na wewe inaitwa Sheria ya Marekebisho ya Walemavu ya Amerika (ADA). Ni sheria ambayo serikali kuu ya Marekani iliunda ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanatendewa kwa haki. ADA inazuia ubaguzi kwa misingi ya ulemavu kama sheria zingine za haki za raia zinavyozuia ubaguzi kwa misingi ya rangi, jinsia, asili ya kitaifa, umri, na dini. ADA inahakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata fursa sawa na wengine katika ajira, kununua bidhaa na huduma, na kushiriki katika programu za serikali za jimbo na za mitaa.

Ikiwa unahisi kama mtu fulani hakutendei wewe au mtoto wako mwenye ulemavu kwa haki au mtoto wako anatendewa kujeruhiwa au kuonewa, unaweza kupiga nambari hii kwa usaidizi:

Mstari wa Habari wa ADA: 1 (800) 514-0301 au 1 (833) 610-1264 (TTY)

- Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Ijumaa, 9:30 asubuhi – 12:00 alasiri na 3:00 alasiri – 5:30 alasiri, Saa za Mashariki (ET)
- Alhamisi, 2:30 alasiri – 5:30 alasiri, Saa za Mashariki (ET)

Community Resources

There are many resources in the community to help you.

Providence Swindell's Family Resource Center supports parents and caregivers of children who have special health, behavioral or developmental needs. You can call them at **1 (833) 868-4769** to get connected to family resources.

Oregon Center for Children and Families with Special Healthcare Needs, Family to Family Health Information Center

The Oregon Family to Family Health Information Center supports families and caregivers of children with special health needs when navigating complex health care systems. Staffed by parents of children and youth with a variety of health conditions, we provide free one-to-one support, training, and printed materials to families and professionals who serve them. This website houses hundreds of resources for parents, grandparents, and youth.

To speak to an OR F2F HIC Parent Partner call **(855) 323-6744**
or email **contact@oregonfamilytofamily.org**

Somali Empowerment Circle

Call (503) 810-8010

Somali Empowerment Circle (SEC) is a small grassroots organization with a mission to promote the mental health and well-being of Somali immigrant and refugee families and youth, improve maternal health and early childhood outcomes, and advocate for safe and affordable housing. SEC aims to empower individuals and communities by providing culturally responsive mental health services, supporting families through the critical stages of pregnancy and early childhood, and advocating for policies that address the root causes of housing insecurity.

African Youth Coalition of Oregon, Bridge to Health Program

Call (971) 254-8916

The African Youth Coalition of Oregon offers health care and disability services aim to BRIDGE the gaps in services experienced by new immigrants. The staff provide knowledgeable guidance through health care and disability resources, with an understanding of the language and culture of those seeking this support.

Rasilimali za Jumuiya

Kuna rasilimali nyingi katika jamii za kukusaidia.

Kituo cha Rasilimali za Familia ya Providence Swindell hutoa msaada kwa wazazi na walezi wa watoto wenye mahitaji maalum ya afya, tabia au maendeleo. Unaweza kuwapigia simu kwa **1 (833) 868-4769** ili kupata mawasiliano na rasilimali za familia.

Kituo cha Habari ya Afya ya Familia hadi Familia cha Oregon kwa Mahitaji Maalum ya Afya, Kituo cha Habari za Afya ya Familia hadi Familia

Kituo cha Habari ya Afya ya Familia hadi Familia cha Oregon kinasaidia familia na walezi wa watoto wenye mahitaji maalum ya afya wanapopitia mifumo ngumu ya huduma za afya. Kikiendeshwa na wazazi wa watoto na vijana wenye hali tofauti za kiafya, tunatoa msaada wa bure wa moja kwa moja, mafunzo, na vifaa vya kuchapishwa kwa familia na wataalam wanaowahudumia. Tovuti hii ina mamia ya rasilimali kwa wazazi, w, na vijana.

Ili kuongea na Mshirika wa Wazazi wa OR F2F HIC piga simu **(855) 323-6744**

au barua pepe **contact@oregonfamilytofamily.org**

African Family Holistic Health Organization (AFHHO)

Piga simu (503) 206-7672

African Family Holistic Health Organization ni shirika lisilo la faida lenye makao yake makuu Kusini-mashariki mwa Portland. Maono yao ni kuboresha maisha ya wahamiaji na wakimbizi huko Portland kwa kupunguza mfadhaiko kwa akina mama wajawazito na kusaidia familia kutumia mfumo wa huduma ya afya. wanatoa mafunzo mahususi ya kitamaduni kabla ya kuzaa kwa akina mama wa Kiafrika, yaliyotafsiriwa katika lugha mbalimbali, kutoa vipindi vya pamoja vya watoto wachanga, usaidizi wa doula na huduma za maendeleo ya mtoto.

IN CLOSING

Hi! Wow! That was a lot of information. We hope all that information was helpful for you. It's very important that we work to support our children and our community. Here are some ways we can be supportive:

Education and Awareness: Let's educate ourselves and others about disabilities, their diversity, and the challenges faced by individuals with disabilities.

Accessible and Inclusive Spaces: Advocate for and actively support accessible spaces, ensuring that mosques, community centers, and public spaces are designed to allow full participation for all, including those with disabilities. Is a sign-language interpreter available for people with hearing impairments? Are community spaces and bathrooms accessible for people who use mobility devices like wheelchairs? Do people with disabilities have an equal opportunity to participate and contribute?

Language Matters: Be mindful of the language we use when talking about disabilities. Sometimes we are not sure of what the appropriate title is for a certain disability or condition, especially in our native tongue, and we use what vocabulary is available to us. Let's be curious, mindful, and creative when attempting to label a disability. What is the name of the disability? How would the individual like to be referred to?

Supportive Networks: To locate all the resources needed for yourself or for your family, it will take collaboration and support from a team. Ask for help when you need it. Offer help when you can! Do your best to share resources and knowledge with your community.

MWISHO

Lo! Hiyo ilikuwa ni habari nyingi sana. Tunatumai kuwa habari zote hizo zilikuwa na manufaa kwako. Ni muhimu sana kwamba tunashirikiana kusaidia watoto wetu na jamii yetu. Hapa kuna njia kadhaa tunazoweza kutowa msaada:

Elimu na Uelewa: Waswahili husema, “Kutokuwepo kwa mwanga ni kutokuwepo kwa maarifa.” Tujitahidi kuelimishana na wengine kuhusu ulemavu, tofauti zake, na changamoto zinazokabiliwa na watu wenye ulemavu.

Nafasi Zinazopatikana na Zenye Kujumuisha: Tangaza na uunge mkono nafasi zinazopatikana, kuhakikisha kuwa misikiti, vituo vya jamii, na maeneo ya umma yameundwa kuruhusu ushiriki kamili kwa wote, ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. Je, kuna mkalimani wa lugha ya ishara anayepatikana kanisani au kwenye mahotuba ya kuhubiri kwa watu wenye ulemavu wa kusikia? Je, nafasi za jamii na vyoo zinapatikana kwa watu wanaotumia vifaa vya kutembea kama vile viti vya magurudumu? Je, watu wenye ulemavu wanayo nafasi sawa ya kushiriki na kuchangia?

Umuhimu wa Lugha: Tuwe makini na lugha tunayotumia tunapozungumza kuhusu ulemavu. Kwa lugha ya Swahili, mara nyingine hatujui ni jina gani sahihi la kutumia kwa ulemavu au hali fulani, hasa katika lugha yetu ya asili, na tunatumia maneno tunayoweza kupata. Tuwe na hamu ya kujifunza, tuwe makini, na tuwe na ubunifu tunapotaka kuelezea ulemavu. Ulemavu huu unaitwaje? Mtu binafsi anapenda kuitwa vipi?

Mtandao wa Usaidizi: Ili kupata rasilimali zote unazohitaji kwa ajili yako au kwa familia yako, itahitaji ushirikiano na msaada kutoka kwa timu. Omba msaada unapohitaji. Toa msaada unapoweza! Jitahidi kushiriki rasilimali na maarifa na jamii yako.

We want you to meet our friend Lilian, who helped us with this book! Here's a letter from her. We hope you enjoyed this book!

Dear Fellow Parent,

As someone who has walked a similar path, I understand the emotional rollercoaster you may be experiencing when facing a potential developmental delay or disability diagnosis for your child. Feeling nervous, uncertain, and overwhelmed by the unknown is completely normal. Please know that you are not alone on this journey.

When I learned of my son's schizophrenia diagnosis, I was engulfed by a storm of emotions. The uncertainty of what lay ahead seemed daunting, but I want to assure you that there is hope. With the right support, resources, and a strong network, our children can exceed our expectations and thrive. Today, I am a proud parent of a child with schizophrenia, whose unique abilities and strengths continue to inspire me.

Throughout my journey, I have discovered the importance of accepting our children as they are and appreciating the beauty and value in every aspect of their lives. They are precious gifts entrusted to us, and we have been chosen because we are the best parents for them. Our role is to celebrate their successes, provide consistent support, and be ambassadors for their growth and achievements.

As we continue on this path together, remember that you are a fantastic role model for your child. Embrace your role with love, patience, and hope. Having witnessed my child blossom and thrive, I am confident that your child can too. Let us come together in solidarity, celebrating the unique individuals our children are and promoting their development in a world enriched by their presence.

With respect and best regards,
Lilian Olero

Tunataka umfahamu rafiki yetu Lilian, ambaye alitusaidia kuandika kitabu hiki! Hapa kuna barua kutoka kwake. Tunatumai umependa kitabu hiki!

Mpendwa mzazi mwenzangu,

Kama mzazi ambaye amepitia njia kama hii, ninajua hali za kupanda na kushuka za kihisia ambazo zinaweza kukupitia unapokabiliwa na uwezekano wa kucheleweshwa kwa ukuaji au utambuzi wa ulemavu kwa mtoto wako. Ni kawaida kabisa kujisikia woga, kutokuwa na uhakika, na kuzidiwa na mambo yasiyojulikana. Lakini tafadhali, fahamu kwamba hauko peke yako katika safari hii.

Niliposikia mtoto wangu mwenyewe aligunduliwa na skizofrenia, nilijikuta nikiwa nimezama katika dhoruba ya hisia. Kutokuwa na uhakika wa kile kilichokuwa mbele kulionekana kulemea, lakini nikuhakikishie, kuna tumaini mbele. Kwa usaidizi ufaao, rasilimali, na mtandao thabiti wa usaidizi, watoto wetu wanaweza kuzidi matarajio yetu na kustawi zaidi ya uwezekano. Leo, ninasimama kwa fahari kama mzazi wa mtoto wa pekee mwenye skizofrenia, ambaye uwezo wake wa kipekee na nguvu zake zinaendelea kunivutia.

Katika safari yangu yote, nimegundua umuhimu wa kuwakubali watoto wetu jinsi walivyo, kuthamini uzuri na thamani katika kila nyanja ya maisha yao. Ni zawadi zenye thamani ambazo tumekabidhiwa, na tumechaguliwa kwa sababu tu sisi ni bora zaidi kwao. Jukumu letu ni kusherehekea mafanikio yao, kutoa msaada thabiti, na kuwa mabalozi wa ukuaji na mafanikio yao.

Tunapoendelea kwenye njia hii pamoja, kumbuka kuwa wewe ni mfano mzuri wa kuigwa kwa mtoto wako. Kubali jukumu lako kwa upendo, subira na matumaini. Kwa kuwa nimeshuhudia mtoto wangu akichanua na kustawi, nina hakika kwamba wako pia anaweza kufanikiwa. Tuungane pamoja kwa mshikamano, tukisherehekea watu wa kipekee ambao ni watoto wetu ni na kukuza maendeleo yao katika ulimwengu uliorutubishwa na uwepo wao.

Kwa heshima na salaam za dhati,
Lilian Olero



This guide was created
for you by:

All:Ready

The All:Ready Network was formed in 2018 in the Portland Tri-County region to re-design our early childhood system of care so that race, class and ability are longer predictors of accessing early childhood resources and services that mitigate adverse health experiences. The Network brings over 60 individuals – Birthing People, Culturally Specific Organization Staff, Community Health Workers, Pediatricians, Maternal Child Health Managers and more – together in Child Success Design Projects and Community Gatherings where we create journey maps, identify gaps in service delivery models, create solutions and recommendations and improve touchpoints in the system that will help create more integrated care.

We were formed thanks to the staff at Health Share of Oregon as part of the Early Life Health portfolio and are currently housed within the Early Childhood Team at Clackamas County's Children, Families and Community Connections.

We express our gratitude for Trillium Community Health Plan, Health Share of Oregon and the Marie Lamfrom Charitable Foundation for the financial support for community engagement, booklet development including translation and cultural adaptation.